# EBU TUONGEE KUHUSU USAWA KATIA HUDUMA ZA MATIBABU

Toleo la 11 OFISI YA USAWA KATIKA HUDUMA ZA MATIBABU
GAZETI LITOLEWALO ELIMU YA AFYA

Usawa katika huduma za matibabu ni kama watu wote wanapata fursa ya kuwa na afya nzuri, hasa watu waliwopitia katika matatizo ya hitilafu, waliowodhulumiwa na waliowopitia kati ya ukosefu wa usawa uliwoweza kuepukiwa, na unawokwenda sambamba na kabila, jinsia, hadhi ya kijamii katika jamii,ubaguzi wa jinsia, na ulemavu.


## AFYA YAKO INAATHIRIWA NA NINI?

**Vipengele vya afya** ni vitu vinavyoweza kutusaidia kuwa na maisha marefu aliyo na afya nzuri. Navyo ni mwenendo wetu uhusikawo na afya, matibabu, vipengele vya kijamii na kiuchumi, na mazingira tuliyo nayo.

**Mienendo ya afya** ni pamoja na kuvuta tumbaku, chakula tunachotumia, mazoezi ya kulegeza mwili, na vitendo vya kuingiliana. Kwa kawaida, tunapendelea kudhibiti mienendo ya afya, kwa kulinganisha na vipengele vingine vya afya. Kurekebisha mienendo ya afya vinaweza kuleta mabadiliko mazuri na matokeo mazuri kwa afya yetu. Lakini kuna vipengele vingine vinavyoathiri chaguo letu kuhusu afya.

**Viamuzi vya kijamii katika afya** ni vipengele vinavyoweza kuathiri afya na mwendo wa afya yako. Vipengele hivi vinaathiri sana afya na vinabadilishiwa kwa kutumia sera, program na uwezo wa serikali.

**Vipengele vya kijamii na kiuchumi** ni pamoja na elimu, kazi, mapato, misada ya kijamii, na usalama wa jamii. **Matibabu ni pamoja na** uwezo wa kufika kwa vituo vya afya, kupata matibabu kama ipasavyo, na uzuri wa matibabu. **Mazingira** ni pamoja na uzuri wa hewa na maji, makazi na uchukuzi. **Vipengele hivi vyote vinaweza kuathiriwa na sera, program na uwezo wa serikali.**




# VIAMUZI VYA AFYA

## VITU VILIVYO NA UWEZO

### UTHABITI WA UCHUMI

- Ufukara
- Uthabiti wa makazi
- Kasi
- Utoshelevu wa chakula & Njaa
- Uchukuzi/usafiri
- Gharama za matibabu
- Gharama & mikopo



### ENEO YA MAKAZI NA MAZINGIRA YALIYOJENGWA

- Zip Code & Jiografia
- Makazi ya bei rahisi & makazi mazuri
- Uwezo wa kupata chakula bora
- Uharibu & Vurugu
- Mazingira ya mimea aliyo salama & viwanja vya michezo
- Hali ya hewa & Maji safi
- Uwezo wa kutembea na miguu& Njia za wanawotumia miguu
- Ukosefu wa maduka ya vyakula
- Ukosefu wa vituo vya matibabu
- Uwezo wa kusafiti

### MFUMO WA HUDUMA ZA TIBA

- Uwezo wa kufika kwa vituo vya huduma za matibabu
- Uwezo wa kufika kwa mgamga wa familiya & kwa mhudumu wa tiba anayeaminiwa
- Huduma bora za matibabu
- Kuelewa maelezo ya afya ya msingi
- Uwezo wa kupata huduma za afya
- Kuelewa utamaduni na lugha
- Kuelewa huduma za matibabu ya waliwopatwa na kiwewe

Taarifa kutoka kwa Sehemu ya Afya ya Serikali ya New York, " Sehemu 6 za viamuzi vya afya katika jamii".

# KATIKA JAMII

## WA KUATHIRI AFYA YAKO



### KUPATA HUDUMA ZA LUGHA

- Tafsiri
- Huduma za ukalimani
- Ujuzi wa maelezo ahusikayo na afya
- Uwezo wa kusoma na kuandika
- Mitandao ya teknolojia na tafsiri itumiyayo simu
- Kuelewa jinsi huduma za matibabu zinagharamiwa

### MAZINGIRA ANAYOSHIRIKISHA JAMII

- Misada kutoka kwa jamii
- Kutengwa & Kushirikishwa
- Kiwewe
- Mfadaiko utokanawo na shida
- Uwezo wa jamii
- Ubaguzi wa kabila & ukandamizaji
- Ubaguzi & ukosefu wa usawa
- Alama ya fedheha
- Kufungwa jela
- Kurasimisha

### ELIMU

- Elimu ya watoto wadogo & ukuaji
- Elimu ya sekondari juu
- Kuandinkwa katika chuo kikuu
- Lugha & mafunzo ya kusona/kuandika
- Ukuaji wa wafanyakazi
- Uzoefu kazini
- Elimu rasmi
- Kazi &ufundi
- Mazoezi ya ufundi & ufundi uliwofundishwa

# USAWA KATIKA MATIBABU NI NINI?



## USAWA NA KUTENDEWA HAKI

Kwa kuelewa usawa katika huduma za afya, tunalazimishwa kwanza kuelewa hitilafu iliyopo kati ya usawa katika huduma za afya, na kutendewa sawa sawa na watu wengine. Foundation ya Robert Wood Johnson inatusaidia hapa chini kuelewa hitilafu za msingi kati ya mambo haya mawili. Usawa ni ni kumtibu kila mtu kama unavyomtibu mtu wowote. Wakati kumtendea haki kimatibabu ni kumtibu mtu kwa aina ya tiba anayohitaji kwa hali ya afya aliyo nayo.

**EUSAWA:**
Kila mtu anatibiwa sawa sawa, bila kujali kama anahitaji yale matibabu au kama matibabu haya atamsaidia mtu huyu.



**KUTENDEWA HAKI KIMATIBABU:**
Kila mtu anapewa matibabu anayohitaji – kwa kuelewa vizuizi, hali na mazingira yake.



Copyright 2022 Robert Wood Johnson Foundation

## MATOKEO KWA AFYA

Kufanya afya iwe nzuri zaidi ni sehemu muhimu ya matibabu anayozingatia vizuizi, hali na mazingira ya mgonjwa. Matokeo kiafya anapima jinsi ya kuingiliya kati kwa kumpima mgonjwa au kumupa elimu, vinaweza kufanya afya kuwa nzuri zaidi kwa mtu au kwa jamii. Matokeo mazuri kwa afya kwa mtu binafsi inaonesha kuwa iko na afya nzuri – kama anashinda bila kulazwa hospitalini au bila kuumia mwilini –au matokeo mabaya kiafya kama kuwa mgonjwa au kuaga dunia akiwa na umri mdogo wa miaka. Urefu wa maisha yako na hali ya afya yako ni matokeo muhimu ya afya. Matokeo ya afya anakwenda sambamba na vipengele vya afya, kama viamuzi vya kijamii katika afya.

### AINA YA KUINGILIA KATI KIMATIBABU

- **Kuwafikia kwawo –** na kuchangia taarifa na watu waliwo na mahitaji ya kujua
- **Kupima –** kupima watu waliwo na magonjwa
- **Elimu ya majonjwa ya mlipuko na Uchunguzi –** kufanya utafiti ili kujua ni watu wangapi wanawoishi na magonjwa gani na namna magonjwa haya anasambaa katika jamii.
- **Elimu ya afya –** kuwafundisha jamii elimu ya magonjwa, na jinsi ya kubakia na afya nzuri
- **Kuleta elimu ya afya sokoni** – kuunga mkono mazowezi anayozuia ujonjwa kujitokeza.
- **Kuleta sera mpya –** kubadilisha namna tunaunga mkono jitihada za kuzuia ugonjwa katika jamii.

# UNATENDEWA KAMA UNAVYOHITAJI KIMATIBABU KAMA:



"Kama watu wote wana fursa ya kutibiwa na kuwa na afya nzuri, hasa wale waliwo na hali ngumu kijamii na kiuchumi, waliwo na historiya ya kudhulimiwa na waliwo kati ya hitilafu ya utaratibu iliyoweza kuepukwa, ambayo inakwenda sambamba na kabila, jinsia, msimamo katika jamii,kufanya mapenzi na jinsia yawo, na ulemavu fulandi"

-Kelly Marie Wofford, Kionghozi wa Ofisi ya Wilaya ya Erie inayohusika na Usawa wa huduma za matibabu

Kila mtu anaeishi katika Wilaya ya Erie, anastahili kuendelea ndani na jamii iliyojengwa kwa kumsaidia kuwa na afya nzuri. Inamaanisha kuwa ana afya nzuri nyumbani, mahali pa kazi, katika mashule, vitongoji na mazingira aliyo salama na asiyo na hali wanapoweza kuumiya. Sheria, sera na jinsi ya kuchunga watu vinaweza kuunda hali mbaya itakayo kuwa chanzo cha afya mbaya.

## KIHISTORIA

**SERA, PROGRAM NA UWEZO WA SERIKALI** — KUUNDA → **HITILAFU KATI YA YA MAZINGIRA TULIPOZALIWA, TUNAPOINSI, TUNAPOTUMIKIA, TUNAPOCHEZEA, TONAPOHUDHURIA IBADA NA MAHALI TUNAPOINGILIA KWA UMRI WA UZEE** — KUSABABISHA → **WATU WENGI ZAIDI WANA MATOKEO YA AFYA MABAYA**

## *WAKATI USAWA KATIKA MATIBABU UNATENDEWA*

**SERA, PROGRAM NA UWEZO WA SERIKALI VINAVYOUNGA MKONO** — KUUNDA → **JAMII NA VITONGOJI VILIVYO BORA TULIPOZALIWA, TUNAPOISHI, TUNAPOTIMIKIA, TUNAPOCHEZEA,TONAPOHUDHURIA IBADA, NA TUNAPOFIKIA UMRI WA MIAKA YA UZEE** — KUSABABISHA → **WATU WENGI ZAIDI WANA MAISHA MAREFU NA WANAPOISHI WAKIWA NA AFYA NZURI.**

Kwa mfano, wakati usawa katika matibabu unatendewa,sera na programu vyetu kuhusu chakula vinakutana na watu mahali walipo. Sera na programu hizi zinaungwa mkono na halmashauri ya sera za chakula, motisha kwa maduka ya vyakula milo ilioagizwa na waganga kwa vituo vya matibabu, mfumo wa kubadilishana vitu kwa wakulima wadogo, ugawaji wa chakula kutokana na eneo tofauti, vyakula vilivyo na rutuba wakati maisha amo hatarini, vyakula vinavyozoelewa kitamadhuni, chakula bora na huru shuleni, ulinzi kwa mashamba ya umma, kupanua mkoba wa fedha unawogharamia SNAP, na vingine vyo. Sera na program hizi zinaunga mkono jamii bora na kuzifanya kuwa imara zaidi kwa ajili ya kuwezesha watu kupata chakula wanachopenda na kinachowafanya kuishi maisha marefu wakiwa na afya nzuri.



“Kama ua linashindwa kujifungua, unatengeneza mazingira ua lilipootea badala ya kuimarisha ua”

-Alexander den Heijer

# MIZIZI YA CHANZO NI IPI?





Mizizi ya chanzo ni vitu vilivyosababisha tatizo kujitokeza au mgogoro unawoonekana katika jamii yetu. Mashirika ya wanawoishi pamoja mara nyingi wanatengeneza sera na sheria zilizo na lengo nzuri, lakini zinashindwa kutatua matatizo aliyopo. Kwa mfano, tunataka kuwa na suluhu yakutatua ishara za ugonjwa wa moyo na kuelewa kwa nini watu wanapatwa na ugonjwa wa moyo. Watu wanapatwa na ugonjwa wa moyo kwa sababu tofauti, zikiwemo hali ya shinikizo, chakula, idadi ya mazoezi ya kulegeza mwili, na jenetiki. Lakini, mara nyingi, kuna mizizi ya matatizo inayosababisha watu wachache kuwa na ugonjwa wa moyo.Mfano: chakula mtu anachotumiya kinaweza kumletea hatari ya kupatwa na ugonjwa wa moyo kwa sababu hana uwezo wa kununua matunda au mboga au kwa sababu anaishi katika eneo ambayo haina duka la vuakula.

Kwa kupunguza idadi ya watu wanawopatwa na ugonjwa wa moyo, lazima tutafute kujua kwa nini watu wanaishi na ugonjwa wa moyo, mizizi ya ugonjwa wa moyo na ishara watu wanaonesha, wakiwa na ugonjwa wa moyo. Inatubidi wote tufanye jitihada za kubadilisha matokeo ya afya hasa matokeo ya idadi ya watu wanaishi na ugonjwa wa moyo.

## “NAWEZA NIKAFANYE NINI?”

Watu wengi wanakubali kwamba kuunda jamii za watu waliwo na afya nzuri ni kitu kigumu. Ukiangalia vitu wyote vinavyohitaji kutengenezwa au kuundwa upya, lengo la usawa katika matibabu linaonekana kama jambo lisilowezekana. Lakini tukikamata jukumu kwa sehemu ndogo ya suluhu, lengo la watu waliwo na afya nzuri katika wilaya ya Erie linaonekana kama rahisi kukamilisha. Soma maelezo kwa ukurasa wa nyuma wa toleo hili ujuwe unaweza kutimiza kitendo gani.

# HITILAFU ZA MATIBABU NI ZIPI?



Hitilafu katika huduma za matibabu ni hitilafu zinazoweza kuepukwa kwa kuangalia sababu gani watu wanapatwa na ugonjwa, na kwa nini wagonjwa wanakuwa kwa hali mahututi, baada ya kupatwa na magonjwa. Hitilafu katika afya zinapatikana kwa sehemu za code ya posta, kabila, umri wa miaka, kupendana wakiwa na jinsia moja, hali ya mapato na msimano katika jamii, kuwa alihudhuria masomo hadi darasa gani, na vingine vyo.

Sera na program zina uwezo wa kupunguza hitilafu katika huduma za matibabu. Kwa mfano: tango ilionekana wazi kuwa sumu ya absesto ilikiwa mzizi wa matatizo ya afya kwa watoto na watu wakubwa, sera zilianzishwa kwa ajili ya kupunguza mifano ya watu wanawoishi karibu na sumu ya absesto. Sera hizi na programu zilipokazwa, idadi ya watu waliwopatwa na ugonjwa utokanawo na sumu ya absesto ilipunguka. Katika wilaya ya Erie, tuna program tofauti za kuwasaidia watu waliwopatwa na ugonjwa unawozababishwa na sumu ya absesto. Pia, tuna program za kuingilia kati kimatibabu kwa lengo la kupunguza idadi ya watu wanawoishi mahali palipoonekana kuwa na sumu ya absesto.

Leo hii, ugonjwa usababishwawo na sumu ya absesto ni mfano wa hitilafu katika hali ya afya, kwa sababu watu wanawoinshi katika manyumba mapya au watu waliwo na uwezo wa kuondoa sumu ya absesto kati ya nyumba zawo ni watu ambawo kwa kawaida, hawapatwe na ugonjwa. Kuna watu wengi ambawo hawasumbuwi na matatizo ya sumu ya absesto. Wakati huo huo, watu wanawoishi kati ya manyumba aliyojengwa zamani sana na watu ambawo hawana uwezo wa kuondowa sumu ya absesto ndani ya manyumba yawo wanapatwa na magonjwa mara nyingi. Kundi hili ni kundi la wanawoishi kati ya manyumba aliyojengwa kabla ya mwaka 1978, au karibu watu wote wa mjyi wa Buffalo. Watoto wa umri wa miaka chini ya miaka 6, wanawake waliwo na mimba na wahamiaji na wakimbizi wamo hatarini ya kupatwa na ugonjwa usababishwawo na sumu ya absesto kuliko watu wengine. Tatizo hili ngumu linalazimisha kutimiza sheria ya upangaji, kuingilia kati kwa idara ya afya ya umma, kuunga mkono uwongozi wa mashule, kuwafundisha viongozi wa afya ya watoto na viongozi wa jamii, na sera zilizo na lengo za kupunguza sana idadi ya watu wanawoishi katika mazingira aliyo na sumu ya absesto.

**KILA MTU ALIKUA HATARINI KABISA YA KUKAA KWA MUDA KADHAA KARIBU NA SUMU YA ABSESTO** → **HITILAFU: KUNA MAKUNDI YA WATU AMBAWO WAMO HATARINI KULIKO WENGINE, YA KUPATWA NA UGONJWA UTOKANAWO NA KUKAA KWA MUDA KADHAA KARIBU NA SUMU YA ABSESTO**

## KUISHI KARIBU NA SUMU YA ABSESTO

**KUPUNGUZA KIASI CHA WATU KUSHINDA KWA MUDA KADHAA KARIBU NA SUMU YA ABSESTO** → **KUPUNGUZA HALI YA KUTOFAUTIYANA KABISA**

**Miaka ya 1980**
Sheria ya muungano inaweka vikomo kwa sumu ya absesto ndani ya petroli

**Miaka ya 1990**
Petroli iliyo na sumu ya absesto ilipigwa marufuku na sheria mpya ya muungano inalazimisha wenye manyumba ya kukodi kutangazia wapangaji na wanunuaji habari walizo nazo kuhusu kiasi cha sumu ya absesto na hatari yake katika manyumba yawo.

**Miaka ya 2000**
Fedha za serikali ya muungano zinagharamia program za Wilaya za kuzuia sumu ya absesto, na kuunga mkono familiya zinazokabiliyana na matatizo ya kukaa kwa muda kadhaa nyumbani karibu na sumu ya absesto.

**2018**
Kikosi cha Wilaya ya Erie cha kupambana na sumu ya absesto kimeundwa kwa ajili ya kuunga mkono programu za kuzuia uambukizaji wa sumu ya absesto

## SHERIA YA 2021 YA WILAYA YA ERIE IHUSIKAYO NA USAWA KATIKA HUDUMA ZA AFYA


Sheria ya 2021 ya Wilaya ya Erie ihusikayo na usawa katika huduma za afya iliunda ofisi ya usawa katika huduma za afya kwa lengo la kuimarisha, kutoa elimu na kupanga matokeo mazuri ya afya kwa watu wa usuli ngumu, ikiwemo wala si wawo pekee,- watu wa kabila za wachache, pamoja na watu wa sehemu za mashambani. Kazi ya ofisi ya usawa katika huduma za afya ni pamoja na:

- Kuchunguza na kuelewa hitilafu katika huduma za afya kwa watu wa usuli ngumu na watu waliwoachiliwa pembeni katika wakazi wa Wilaya ya Erie
- Kuelewa na kuunganisha pamoja vitu vya asili vinavyosababisha matokeo ya afya, ikiwemo mazingira, viamuzi vya kijamii vinavyoathiri afya, uwezo wa kupata tiba ya kliniki na mwenendo usababishwawo na afya.
- Kufanya pendekezo kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya kwa wakazi wa Wilaya ya Erie waliwo katika hali ngumu na waliwoachiliwa nyuma.
- Kuongoza maprogramu za kupunguza hitilafu katika huduma za tiba;
- Kukuza fahamu katika jamii na kuratibu sherehe za elimu zinazounga mkono hali nzuri ya afya katika jamii zizoachiliwa nyuma
- Kutangaza ripoti zinazoeleza hitilafu kati ya wakazi watokawo katika makabila za waliowachache na makundi ya wanawopendana wakiwa kwa jinsia kama yawo, katika Wilaya ya Erie.
- Kufanya kazi pamoja na sehemu na mashirika aloyo na lengo la kupunguza hitilafu katika huduma za afya

Soma sheria hapa: erie.gov/heact

# KAMATA HATUA

## NJIA YA KUIMARISHA USAWA KATIKA HUDUMA ZA AFYA KATIKA JAMII YAKO




CHANGIA TAARIFA | JIANDIKISHE KATIKA DARASA | JISHIRIKISHE KATIKA UCHUNGUZI | TETEA | SWALI | TOA MUALIKO

Unaweza kuunga mkono usawa wa huduma za afya katika jamii yako, kwa hatua chache zilizo rahisi. Changiya habari kuhusu usawa katika huduma za afya na washiriki, warafiki na na majirani. Toleo hili ni mahali pazuri pa kuanzia. Jiandikishe kwa mafunzo ya kuongeza elimu yako kuhusu usawa katika huduma za afya au ya kuunga mkono jitihada za kupunguza hitilafu katika huduma za afya. Jishirikishe katika uchunguzi wa huduma za afya na uchunguzi katika jamii. Ni kitu muhimu kwa uchunguzi kupata majibu kutoka sehemu mbalimbali za Wilaya yetu. Kutetea watu wengine. Ndani ya kituo cha kazi, unaweza kumomba mwajiri kuimarisha sera zihusikazo na kutambua jinsia. Kuonesha wasiwasi juu la sera na program zinazotenga makundi au zinazoshindwa kusimamia mahitaji ya kila mtu. Kama uko kwa cheo chilicho na malmaka, toa mualiko kwa makundi mengine kwa meza. Usawa katika huduma za afya unatubidi wote kushiriki.

***HII NI GAZETI YA OFISI YA***

**WILAYA YA ERIE IHUSIKAYO NA USAWA KATIKA HUDUMA ZA AFYA**

**Gazeti hili linapatikana kwa lugha 5 za nyongeza**

Maoni ya Wilaya ya Erie, Usawa wa Huduma za Afya ni kuona kila mtu katika Wilaya ya Erie anatimiza hali nzuri ya afya. Ofisi ihusikayo na usawa wa huduma za afya inahifadhiwa ndani ya Sehemu ya Afya ya Wilaya ya Erie.

***Unataka kujuwa zaidi?***

Tembeleawww.erie.gov/health-equity

Tuandikie baruwa pepeHealthEquity@erie.gov

Erie County Department of Health

Public Health Prevent. Promote. Protect.

**OFISI YA USAWA KWA HUDUMA ZA AFYA**

**www.erie.gov/health-equity**

Rev. 01.2024